



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU



TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MTIHANI WA PAMOJA WA KISWAHILI

KIDATO CHA TATU

O21

MUDA : SAA 3

MWAKA 2026

MAELEKEZO


MsomiBora.com

- Mtihani una
- Jibu maswali yote katika sehemu A na B na maswali mawili katika sehemu C na swali la 9 ni la lazima.
- Zingatina maelekezo ya kila sehemu na ya kila swali.
- Majibu yaandikwe kwa kalamu yenye wino wa **bluu** au **mweusi**.

SEHEMU A.(ALAMA 16)

1. Jibu maswaliyote katika sehemu hii;

- Anatoa ufafanuzi juu ya ubantu wa Kiswahili kwa kuelezea wakati wa mwambao waliojulikana kama “Wazanji” na watawala wao kama “wakilini”
 - Ali – idris
 - Marcopolo
 - Ibin batuta
 - Morice
 - Al – masudi
- Chagizo katika uchanganuzi wa sentensi hutumika katika mkabala wa
 - Kimuundo

- 
- (b) Kisasa
(c) Kimapokeo
(d) Kisintaksia
(e) Kimambo leo
- (iii) Maneno yafuatayo yana maana zaidi ya moja isipo kuwa
(a) Ua
(b) Mbuzi
(c) Kata
(d) Nyau
(e) Paa
- (iv) Vipengele vifuatavyo hutumika katika uandishi wa barua pepe isipokuwa;-
(a) Saini
(b) Anuani ya mwandishi na mwandikiwa
(c) Lengo
(d) Jina la mwandishi
(e) Mada au kichwa
- (v) Bata anapenda maji machafu. Neno lililopigiwa mstari lipo katika ngeli ipi?
(a) I – ZI
(b) KI – VI
(c) KU
(d) YU – A – WA
(e) LI – YA
- (vi) Ni jambo gani linadhihirisha upekee wa kazi ya kifasihi?
(a) Wahusika wa kazi husika
(b) Msimamo wa kazi husika
(c) Falsafa ya kazi husika
(d) Muundo wa kazi husika
(e) Mtindo wa kazi husika

- (vii) Neno ngeli asili yake ni lugha ya
- (a) Kipare
 - (b) Kizaramo
 - (c) Kihaya
 - (d) Kimeru
 - (e) Kingoni
- (viii) Nifungie zege mbili zilizokauka vizuri. Hii ni rejesta ya mahali gani
- (a) Mtaani
 - (b) Sokoni
 - (c) Mgahawani
 - (d) Shambani
 - (e) Mafundi ujenzi
- (ix) Lahaja ya kintang'ata huongelewa sehemu gani ya pwani ya Afrika mashariki?
- (a) Kigoma
 - (b) Kisiwa cha mafia
 - (c) Pwani ya Somalia
 - (d) Kisiwa cha unguja
 - (e) Kaskazini mwa pwani ya Tanga.
- (x) Mama Fatuma hupenda kusimulia hadithi kuhusu vita vya majimaji. Je hizi ni aina gani za hadithi?
- (a) Ngoma
 - (b) Hadithi
 - (c) Vigano
 - (d) Visasili
 - (e) Tarihi

2. Oanisha maelezo yaliyopo katika orodha A na dhana zilizopo katika orodha B, kisha andika herufi ya jibu sahihi katika kijitabu chako cha kujibia.

KIFUNGU A	KIFUNGU B
(i) Utata (ii) Lahaja (iii) Ramsa,tanzia, vichekesho (iv) Chagizo (v) Sentensi changamano (vi) Simo	A. Mafia, unguja,pemba B. Mkondo wa hadithi za fasihi andishi C. Huundwa na KN, KT, KE D. Huundwa na Khr na Ktg E. Kinzuani, chimiini, kingao F. Mikondo ya hadithi G. Hutumia lugha ya kifasihi H. Mikondo ya tamthiliya I. Ni hali ya neno au sentensi kuwa na maana zaidi ya moja J. Maneno yasiyo sanifu yanayoanzishwa na kikundi cha watu Fulani wenye utamaduni mmoja K. Tofauti za kimatamshi na kimsamiati za lugha moja zinazojitokeza kulingana na maeneo ya kijiografia L. Kikundi cha maneno kinachojaza M. Nafasi ya kielezi katika tungo.

SEHEMU B (ALAMA 54)

3. (a) Ainisha viambishi vya neno “Vimeshikamana” kisha bainisha jukumu la kila kiambishi kama kinavyotumika.
(b) Uandishi wa barua, hususani barua za kirafiki na rasmi, unakabiliwa na changamoto kubwa katika jamii ya kisasa. Bainisha changamoto hiyo na utoe sababu mbili zinazochangia.
4. Ubuntu wa Kiswahili unaonekana kuwa na mashiko zaidi ukilinganisha na nadharia nyingine zinazoelezea chimbuko au asili ya kiswahili. Ukiwa kama mwanaisimu wa lugha, thibitisha ukubalifu wa nadharia ya ubuntu kwa hoja tano za kiisimu.
5. (a) kishazi tegemezi hutoa taaarifa isiyojitosheleza na hutegemea kishazi huru ili kukamilisha taarifa yake. Kwa mifano bainisha maumbo yanayounda kishazi tegemezi hoja tatu.
(b) Sentensi sahili imeundwa kwa njia tofauti tofauti, fafania kwa mifano miundo mitatu ya sentensi sahili.
6. (a) Andika visawe vya maneno yafuatayo kisha tunga sentensi moja kwa kila sentensi
(i) Simu
(ii) Chuchumaa
(iii) Sifuri
(b) Upatanisho wa kisarufi ni kigezo kimoja wapo kati ya vigezo vya kuunda ngeli za nomino. Thibitisha dai hili kwa kutunga sentensi mbili katika kila ngeli zifuatazo;-
(i) Ngeli ya pili

(ii) Ngeli ya nne

7. (a) Uchanganuzi wa sentensi kwa kuzingatia mkabala wa kimapokeo (kidhima) huzingatia hatua binafsi. Kama mtaalamu wa Kiswahili, taja hatua hizo.
- (b) Changanua sentensi ifuatayo kwa kuzingatia mkabala wa kidhima. “Juma anapika ugali vizuri”
8. Wewe ni mwanafunzi wa kidato cha tatu. Umechaguliwa kuwa katibu wa kikao cha kupanga mahafali ya kumaliza kidato cha nne. Andika kumbukumbu ya kikao kilichofanyika shuleni kwako tarehe 08/08/2026 kilichokuwa na wajumbe kumi (10).

SEHEMU C (ALAMA 30)

Jibu maswali mawili (02) toka sehemu hii.

Swali la 9 ni la lazima

9. Wasani wengi huweza kujenga vipopo vya kutosha katika kazi zao. Jadili kauli hii kwa kutumia riwaya mbili ulizosoma kwa hoja tatu kwa kila kitabu.
10. Maisha ya mwanadamu ni sawa na “chungu tamu” fafanua mchango wa uchungu uliooneshwa katika tamthiliya na eleza jinsi unavyokusaidia katika maisha yako ya kila siku. Toa hoja tatu kwa kila tamthiliya
11. Waandishi wa ushairi wa Kiswahili hutumia dhamira mbalimbali kuonya, kuelimisha na kuikosoa jamii yao kutokana na changamoto ya

kiuchumi na kijamii. Ukitumia diwani mbili ulizosoma, thibitisha kauli hii, kwa kutoa hoja tatu kwa kila kitabu.

